# Misingi Mikuu ya Utawala kwa Kila Kamati ya Shule




hakielimu

# Misingi Mikuu ya Utawala kwa Kila Kamati ya Shule:

## haki za binadamu
## ushiriki
## uwajibikaji
## uwazi
## demokrasia

hakielimu

| | |
|---|---|
| Waandishi: | Rakesh Rajani, Mary Nsemwa na Godfrey Telli |
| Wachangiaji: | Japhet Makongo, Lilian R. Kallaghe na Kathy Relleen |
| Mhariri: | Rakesh Rajani |
| Mfasiri: | Rogers Cidosa na Godfrey Telli |
| Katuni: | Sammy Mwamkinga |

© HakiElimu 2003/2004
SLP 79401, Dar es Salaam, Tanzania
info@hakielimu.org, www.hakielimu.org

Sehemu yoyote ya kijitabu hiki inaweza kunukuliwa na kuchapishwa tena kwa minajili isiyo ya kibiashara; ilimradi inaelezwa wazi kuwa chanzo cha taarifa hiyo ni kijitabu hiki na kwamba nakala mbili za chapisho hilo zinatumwa kwa HakiElimu.

ISBN 9987 – 8943 – 3 –X

# Yaliyomo

**Dibaji** . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . **i**

Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

**Utangulizi** . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . **1**

**Kamati za Shule na Demokrasia** . . . . . . . . . . . . . . . . . . **2**

Mipango na Programu za Maendeleo ya Elimu nchini Tanzania
Mahusiano na Nafasi yake katika Elimu

**Misingi Mikuu kwa kila Kamati ya Shule:**

Haki za binadamu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 6
Ushiriki . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 9
Uwajibikaji . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 13
Uwazi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 16
Demokrasia . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 20

**Hitimisho** . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . **24**

**Vyanzo na Machapisho Mbalimbali** . . . . . . . . . . . . . . . . **26**

# Dibaji

Serikali inasisitiza kuleta maendeleo na haki kwa ushiriki wa wananchi. Suala hili ni muhimu hasa katika ngazi ya jamii ambapo ndipo wananchi wanapoishi. Ushiriki ni nguzo muhimu katika Programu ya Uboreshaji ya Serikali za Mitaa inayotekelezwa na Serikali.


Elimu ni moja ya sekta muhimu zaidi ya maendeleo. Kijitabu hiki kinaelezea misingi mikuu ya kuongoza kamati za shule na wajumbe wake. Lengo ni kusaidia jitihada za Serikali kuimarisha kamati za shule na kupanua njia ambazo wananchi wanaweza kuchangia kuboresha elimu.

Misingi ya ushiriki katika kamati za shule ni haki za binadamu, ushiriki, uwajibikaji, uwazi na demokrasia. Ni muhimu kwa kila kamati ya shule kuijadili na kuielewa vyema misingi hii ili kuwa na ufanisi zaidi. Naamini kwamba kwa kuzingatia misingi hiyo kamati zitajenga imani kwa wananchi zinaowawakilisha.

Walengwa wakuu wa kijitabu hiki ni kamati za shule za msingi, viongozi wa mitaa na vijiji na shule za msingi. Tunategemea viongozi wa Serikali katika ngazi za mikoa na wilaya kote nchini watafanya jitihada za kuhakikisha kijitabu hiki kinasambazwa na kuwafikia walengwa wote.

Tunatarajia kuwa kijitabu hiki kitakuwa na manufaa kwa jamii. Kitatumika kukuza ufahamu wa wananchi na kuwafanya wachukue hatua zinazostahili kujiletea maendeleo yao.

Jukumu la Serikali ni kuunda sera na kuandaa miongozo ya kuleta maendeleo. Ni jukumu la kila kiongozi na kila mwananchi kutekeleza hayo kwa vitendo.



D. M. S. Mmari
Katibu Mkuu
Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
15 Julai 2004

# Utangulizi

**Utawala bora pia ni kupanua uhuru wa Wananchi – Uhuru wa maoni uhuru wa kuchangia mawazo kuhusu hatma ya jamii uhuru wa kudai uwajibikaji wa viongozi kwa wananchi uhuru unaoimarishwa kwa elimu….”**

**(Rais Mkapa, 31 Mei 2001)**

Kwa mujibu wa sheria, kila shule ya msingi nchini Tanzania inatakiwa isimamiwe na kuendeshwa na kamati ya shule. Kijitabu hiki kinalenga kusaidia jitihada za Serikali katika kuimarisha kamati za shule na kupanua njia ambazo wananchi wanaweza kuchangia katika kuboresha elimu.


Kijitabu hiki si muongozo wa namna ya kuendesha kamati za shule. Hakionyeshi nafasi, wajibu, kanuni na taratibu zote zinazohusika katika uendeshaji wa kamati za shule. Badala yake, kinaelezea misingi mikuu ambayo itaongoza kamati za shule na wajumbe wake. Misingi hiyo ni haki za binadamu, ushiriki, uwajibikaji, uwazi na demokrasia. Ni muhimu kuijadili na kuielewa vyema misingi hii, kwa sababu kamati yoyote ya shule itakayoshindwa kuizingatia itashindwa kuwa na ufanisi, na hivyo kujiweka katika hatari ya kupoteza imani yake kwa wananchi.

Kijitabu hiki kimegawanyika katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza inatoa kwa muhtasari maelezo kuhusu mageuzi ya elimu na nafasi ya kamati za shule katika jitihada za kujenga demokrasia Tanzania.

Sehemu ya pili inaangalia misingi mikuu. Maelezo mafupi yanatolewa kuhusu kila msingi ili kubainisha msingi huo unamaanisha nini na haumaanishi nini. Aidha, maelezo yanatolewa kuhusu umuhimu wa msingi huo katika elimu pamoja na kutoa mawazo mbalimbali kuhusu mambo halisi ambayo wananchi wanaweza kuyafanya katika kuboresha hali iliyopo. Maelezo kwa kila mjadala yanahitimishwa kwa maswali yanayolenga kuchochea tafakuri ya kina na kuibua mjadala kuhusu masuala yaliyojitokeza.

Tunatarajia kuwa kijitabu hiki kitakuwa na manufaa kwako. Kitumie kuchochea na kuibua mijadala na midahalo itakayosaidia kukuza ufahamu wa watu na kuwafanya wachukue hatua zinazostahili. Hebu jiulize: Je kamati ya shule yangu inatekeleza misingi hii? Ninaweza kufanya nini ili kuiboresha? Jadili mawazo na maoni yako na wengine. Wasiliana na viongozi wa serikali ya mtaa au kijiji na wale wa mashirika yasiyo ya kiserikali katika eneo lako. Vilevile tungependa kusikia mawazo na maoni yako. Tafadhali tuandikie kwa kutumia anuani iliyopo nyuma ya kijitabu hiki. Mawazo yako ni muhimu!

# Kamati za Shule na Demokrasia





Mabadiliko yanatokea katika elimu nchini Tanzania! Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) umeleta uhai, mawazo na rasilimali mpya katika shule.  Watoto wengi wapo shuleni. Madarasa mengi yamejengwa. Na ahadi zimetolewa za kuinua ubora wa elimu.

Mabadiliko katika elimu hayako tofauti na mabadiliko mengine yanayotokea nchini. Mageuzi katika elimu ni sehemu tu ya mabadiliko makubwa katika maendeleo ya taifa  na serikali za mitaa, hasa katika maamuzi na matumizi ya rasilimali.

Kuna misisitizo mkubwa katika suala la ushiriki wa wananchi na kuwajibika kwao. Serikali "inakasimu na inapeleka" sehemu kubwa ya mamlaka na rasilimali zake karibu zaidi na wananchi na serikali zao za mitaa. Wazo la msingi hapa ni kuwa watu huhudumiwa vyema zaidi pale ambapo wao wenyewe wanasimamia maendeleo yao.

Mkakati wa Kuondoa Umasikini (MKU), ambao ndio unaotoa mwelekeo wa jumla wa kisera kwa taifa letu, una lengo muhimu la kukuza ushiriki wa wananchi katika michakato ya kisera. Aidha, Sera ya Programu ya Uboreshaji wa Serikali za Mitaa inaeleza kuwa mojawapo kati ya malengo makuu ya mabadiliko haya ni "maendeleo ya kidemokrasia ya jamii kutoka katika ngazi ya jamii" (uk.15).




Lengo la Serikali la kupanua ushiriki wa kidemokrasia na uwajibikaji katika ngazi zote unahitaji ushiriki wa wanaume, wanawake, vijana na watoto katika shughuli za shule. Aina ya uongozi nayo pia inatakiwa kubadilika. Viongozi wa jamii wanatakiwa kuona nafasi na wajibu wao kuwa ni kuwasikiliza na kuwahudumia watu na kwamba wanawajibika kwanza kwa wananchi, siyo tu kutekeleza maelekezo kutoka Serikali Kuu.

Kufufuliwa kwa mabaraza ya vijiji ni mkakati muhimu katika kujenga demokrasia katika ngazi ya jamii. Jitihada za kuongeza sauti na nguvu za kamati za shule zinatarajiwa kuongeza uwajibikaji wa serikali za vijiji na mitaa kwa wananchi.

Mabadiliko katika elimu yamekuwa yakiendeshwa katika mazingira haya haya. MMEM ni mpango wa miaka mitano (2002-2006) unaolenga kuhakikisha kuwa kila mtoto nchini Tanzania anapata elimu bora ya msingi. Vipengele vyake vikuu vinne ni:

- kuongeza uandikishaji wa watoto shuleni
- kuongeza ubora katika ufundishaji na mchakato wa kujifunza
- kujenga uwezo katika mfumo wa elimu
- kuimarisha mifumo ya kitaasisi inayosaidia utayarishaji wa mipango na utoaji wa huduma za elimu.

Mkakati mkuu wa MMEM ni kuboresha elimu kwa kuboresha utawala. Hii inahusisha kujenga mahusiano na ushirikiano wa karibu zaidi kati ya walimu, wanafunzi, wazazi, serikali za vijiji na mitaa na jamii kwa ujumla ili kuimarisha menejimenti ya shule. Lengo kuu ni kukuza ushiriki, demokrasia, uwazi na uwajibikaji katika utawala wa shule.

Mambo haya yanaelezwa katika kiambatanisho cha MMEM cha *Uimarishaji wa Taratibu za Kitaasisi*. Nafasi na wajibu wa ngazi mbalimbali unaelezwa (angalia ukurasa unaofuata). Msisitizo maalumu umewekwa kwamba kamati za shule ndizo zenye jukumu muhimu katika MMEM. Kwa kupitia kamati hizi ndipo wananchi wanaweza kushiriki kikamilifu na kuwa na sauti kuhusu namna ambavyo shule zinaendeshwa. Serikali inakusudia kutoa rasilimali ya fedha na watendaji ili kujenga uwezo wa kamati za shule katika kusimamia na kuendeleza shule.

Chini ya MMEM, kamati za shule zinatakiwa kuandaa "mipango ya jumla ya maendeleo ya shule" na kusimamia bajeti za shule. Mipango hii inakusudiwa kuziwezesha shule kufanya maamuzi kuhusu maendeleo yao. Hii inaiwezesha kila shule kutumia ujuzi na utaalamu uliopo miongoni mwa wanajamii, wanafunzi na walimu kuamua kuhusu mambo yatakayowafaa zaidi. Vilevile, itawezesha uchangiaji na upashaji habari kwa kila mmoja, jambo ambalo litawapa nafasi zaidi ya kufuatilia na kuhakikisha uwajibikaji katika rasilimali na hivyo kuhakikisha ubora katika huduma zinazotolewa.

# Muundo wa Kitaasisi kwa ajili ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Elimu na MMEM

**Kamati ya Uendeshaji**
**Program ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu**

**Kamati ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi (BEDC)**
*Kuandaa sera, kufuatilia na kutathmini maendeleo. Kuwashirikisha na kuwasiliana na wadau wote*

**Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI)**
*Kuongoza na kusimamia utoaji wa elimu ya msingi (Mamlaka za Serikali za Mitaa)*

**Sekretariet ya Mkoa**
*Kusaidia TAMISEMI na kusimamia/kuratibu Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kutoa mwongozo (ushauri) na msaada wa kiufundi.*

**Mamlaka za Serikali za Mitaa (Halmashauri za Wilaya)**
*Kutekeleza MMEM katika maeneo yao na kusimamia na kuratibu Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kutoa mwongozo na msaada wa kiufundi.*

**Kamati ya Maendeleo ya Kata**
*Kusaidia uendeshaji wa shule*

**Baraza la Kijiji/Mtaa**
*Kuhamasisha jamii ili kuunga mkono na kuisaidia MMEM, kusimamia kamati za shule ili kuhakikisha kuwa zinashughulikia kero zilizopo na zinawajibika ipasavyo. Kuongeza upatikanaji wa taarifa miongoni mwa wananchi.*

**Kamati ya Shule**
*Kuwa kiungo kikuu na jamii, kuamua na kupanga vipaumbele vya shule. Kusimamia utoaji wa elimu.*

**Uongozi/Menejimenti ya Shule**
*Kuendesha shule na kutekeleza MMEM kwa mujibu wa sera za Serikali na miongozo ya kamati za elimu. Kukuza na kuendeleza uwazi*

**Baraza la Shule/Baraza la wanafunzi**
*Kuwasilisha maslahi ya wanafunzi katika utawala wa shule. Kushiriki katika kuandaa na kufuatilia mipango na bajeti za shule Kusambaza taarifa.*

**Wizara ya Elimu na Utamaduni**
*Kuratibu uwekaji mipango shirikishi, utayarishaji wa sera, kanuni, ufuatiliaji,tathmini, kuhakikisha ubora na kuchangia taarifa*

**Ukaguzi Kanda**
*Kuratibu taratibu za ukaguzi, kutoa miongozo na ushauri wa kitaalamu katika kuhakikisha ubora*

**Ukaguzi Wilaya**
*Kuhakikisha kuwa kila shule inakaguliwa angalau mara moja katika kila baada ya miwili. Kushauri kamati za shule kuhusu utawala wa kidemokrasia. Kujenga uwezo wa wafanyakazi*

*Chanzo: Kiambatanisho cha MMEM – Uimarishaji wa Taratibu za Kitaasisi*

# Haki za Binadamu



## Haki za binadamu ni nini?

- mambo unayostahili kuyapata katika jamii
- ni sehemu ya wewe kuwa mwanadamu,  ni ‘zawadi asilia’
- hupewi na mtu yeyote (na hakuna yeyote anayeweza kukunyang’anya)
- ni kwa ajili ya binadamu wote – masikini au matajiri, wanawake au wanaume – bila ubaguzi
- hazigawanyiki, zote zinakwenda pamoja na zote ni muhimu
- zinathibitishwa katika Katiba na zinatambuliwa na sheria na Serikali

## Nini si haki za binadamu?

- matakwa au matamanio binafsi
- hisani ambayo unaweza kutunukiwa
- majukumu ambayo ni lazima uyatekeleze

## Kwa nini haki za binadamu ni muhimu?

- zinathibitisha utu wako
- zinathibitisha kuwa wewe ni muhimu kama walivyo binadamu wengine wote
- zinamaanisha kuwa unastahili kuheshimiwa na wengine
- zinakulinda dhidi ya unyanyasaji
- zinamaanisha kuwa mawazo na maoni yako ni muhimu na una haki ya kusikilizwa
- zinakujengea uwezo wa kujua nafasi yako katika jamii
- zinakuwezesha kuuliza maswali na kutoa maoni yako
- zinajenga umoja na usawa

## Unaweza kufanya nini kuhusu haki za binadamu?

- jifunze kuhusu haki zako, na wasaidie wengine kujifunza
- soma machapisho na nyaraka muhimu ikiwa ni pamoja na Katiba, Mkakati wa Kuondoa Umasikini (MKU), za MMEM na viambatanisho vyake na za uboreshaji wa serikali za mitaa
- sikiliza vipindi vya redio na televisheni vinavyohusu haki za binadamu
- jadili na wengine kuhusu hali halisi ya haki za binadamu na sera
- andika na changia uzoefu na maoni yako juu ya haki za binadamu

- ongelea na jaribu kuzuia ukiukwaji wa haki za binadamu
- hakikisha vitendo vyako vinaenda sambamba na havikiuki haki za binadamu
- waunge mkono watu wanaopigania haki zao
- toa taarifa kwa mamlaka zinazohusika kuhusu vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu (pale haki zinapovunjwa Serikali inawajibika kuchukua hatua)

**Maswali kwa ajili ya majadiliano**

- Je haki za binadamu zinaheshimiwa katika jamii yako? Katika shule yako?
- Je baadhi ya watu wanabaguliwa zaidi kuliko wengine? Hao ni akina nani? Unaweza kufanya nini ili kuwasaidia?
- Je ukiukwaji wa haki za binadamu unaathiri vipi elimu katika shule yako? Nini kinaweza kufanyika kuhusu hali hiyo?
- Je ni kwa namna gani watu – ikiwa ni pamoja na wanafunzi, wazazi na walimu wanaweza kujifunza kuhusu haki zao?
- Je mamlaka/serikali katika eneo unaloishi inaendeleza haki za binadamu? Inaweza kufanya nini ili kuboresha hali iliyopo?
- Mwananchi wa kawaida anaweza kwenda wapi ili kutoa taarifa kuhusu masuala ya haki za binadamu huku akijiamini kuwa ataheshimiwa?

# Ushiriki




## Ushiriki ni nini?

- kujihusisha kikamilifu na kwa dhati katika jambo linalokuhusu au linalokugusa
- kuchangia mawazo, dukuduku, maoni na mapendekezo
- kuthaminiwa, kusikilizwa na kuchukuliwa maanani
- kupatiwa taarifa na kushirikishwa katika mashauriano
- kuwa na usemi katika ufanyaji maamuzi
- kufanya uchaguzi kuhusu nini cha kufanya

## Nini ambacho si ushiriki?

- amri na maelekezo bila majadiliano
- kuwakilishwa na watu wasiokusikiliza wala kukujali
- mtu mmoja kuamua kuhusu kila kitu, au kiongozi kufanya maamuzi yote
- kubaguliwa au kutengwa kwa maoni ya mtu fulani
- kuwa gizani kuhusu yale yanayofanyika
- kushirikishwa kama hisani au kwa kuwatumia watu kwa malengo binafsi.
- kuombwa au kutakiwa kutoa maoni yako wakati ambapo tayari maamuzi yote yameshafanyika

## Kwa nini ushiriki ni muhimu?

- unawapa watu fursa ya kuchangia mawazo
- unatoa fursa ya kutumia ujuzi na vipaji vya watu
- unaimarisha uwajibikaji na umiliki wa pamoja
- unawapa watu jukwaa la kuchangia maoni na uzoefu
- unaleta ufanisi na uendelevu
- unapunguza rushwa na maamuzi yasiyo ya haki
- unawafanya watu wajisikie vizuri kushiriki

## Unaweza kufanya nini ili kukuza ushiriki?

- chunguza sheria na sera za serikali zinasema nini kuhusu ushiriki na changia taarifa hizo na wengine
- tumia fursa zilizopo kushiriki katika shughuli mbalimbali za shule au jamii kama vile Mkatano Mkuu wa Kijiji/Mtaa (ambapo kila mtu mwenye umri zaidi ya miaka 18 hukaribishwa)

- toa mawazo ya kuboresha hali iliyopo na toa wasiwasi wako pale unapoona watu wananyimwa haki yao ya kimsingi
- tetea haki ya watu ya kupata nafasi au fursa zaidi ya kushiriki, hususan haki za wale ambao kwa kawaida sauti zao hazisikilizwi, mfano, masikini, watoto, wanawake na watu wenye ulemavu
- sikiliza maoni ya wale wanaooathiriwa zaidi na maisha ya shule – wanafunzi, wazazi na walimu – wasaidie maoni yao yaweze kusikilizwa
- tathmini iwapo kamati za shule ni za kidemokrasia katika muundo wa wajumbe wake, katika utendaji wake, na pendekeza njia zinazoweza kutumika ili kuboresha hali iliyopo

## Maswali kwa ajili ya majadiliano

- Je kuna fursa za kutosha za kushiriki katika jamii yako? Katika shule yako?
- Je kuna baadhi ya watu wanaobaguliwa zaidi ya wengine? Hao ni akina nani? Watoto? Wasichana? Watu wenye ulemavu? Watu wanaoishi na VVU/UKIMWI? Unaweza kufanya nini ili kuwasaidia?
- Una mfano mzuri kuhusu ushiriki? Nini kilifanya ushiriki huo kuwa mzuri na ni kwa jinsi gani uliisaidia jamii yako?
- Unafahamu mfano ambapo kukosekana kwa ushiriki kuliathiri maendeleo? Nini kinaweza kufanyika kuboresha hali hiyo?
- Ni mambo gani yanapunguza ushiriki wenye maana? Ni hali gani inatakiwa ili kila mmoja aweze kushiriki kikamilifu?

- Ni kwa namna gani watu katika jumuiya ya shule – wanafunzi, wazazi na walimu wanaweza kushiriki kikamilifu na kwa ufanisi?

- Je serikali inakuza ushiriki? Inaweza kufanya nini ili kuboresha hali iliyopo?

- Je wajumbe wa kamati ya shule yako wanawakilisha maslahi ya kila mmoja katika shule na katika jamii?

- Kamati ya shule yako inaendeshaje shughuli zake? Je sauti ya kila mmoja inasikika kwa usawa?



# Uwajibikaji



## Uwajibikaji ni nini?

- kuwajibika kwa umma na kwa wasimamizi wako wa kazi au wale waliokuchagua kufanya kazi
- kuwajibika kwa matendo na maamuzi yako
- kuwa muaminifu kuhusu mafanikio, changamoto na matatizo au kushindwa
- kukataa kufanya jambo ambalo ni kinyume cha maadili au lisilo sahihi hata kama unashinikizwa kufanya hivyo
- kujali matokeo na kuazimia kupata matokeo mazuri zaidi kutokana na matumizi mazuri na yenye ufanisi ya rasilimali za umma
- kuwa muwazi

## Nini si uwajibikaji?

- kutokuwajibika kwa matendo unayoyafanya au maamuzi unayochukua
- kukwepa kutoa maelezo au kujibu maswali
- kutokutoa mrejesho au taarifa ya utekelezaji kwa wale unaowahudumia au waliokuchagua
- matumizi mabaya ya mamlaka na rasilimali
- kuogopa kuuliza maswali

## Kwa nini uwajibikaji ni muhimu?

- unaboresha ufanyaji maamuzi
- unaongeza heshima, uaminifu na maelewano
- unakuza umiliki wa maamuzi yaliyofikiwa na hatimaye kuleta uendelevu
- unaleta ufanisi katika matumizi ya rasilimali
- unakuza matumizi ya haki ya nguvu na mamlaka
- unasaidia kuepusha uharibifu kabla hali haijawa mbaya zaidi
- unapunguza rushwa, uvunjaji wa sheria na tabia mbaya miongoni mwa viongozi

## Unawezaje kukuza uwajibikaji?


- fahamu haki zako na wajibu wako
- fahamu wajibu wa viongozi kama vile wenyeviti wa kamati za shule, walimu wakuu, madiwani na waratibu wa elimu kata
- tafuta taarifa kuhusu yale yanayotakiwa kufanyika na uliza ni kwa nini hayajafanyika

- waulize viongozi wa shule wakueleze bayana na kwa ukamilifu jinsi rasilimali ikiwa ni pamoja na fedha zilivyotumika na dai taarifa ya kimaandishi
- endeleza utamaduni wa kamati za shule wa kuwashirikisha na kuwasikiliza wananchi kabla ya kufanya maamuzi, na kuwafahamisha wananchi kuhusu maamuzi hayo baada ya kuyafanya
- hakikisha iwapo taarifa zinazotolewa kwako na viongozi ni za haki, sahihi na zenye kukubaliana na sera na ukweli
- toa taarifa kwa mamlaka zinazohusika pale unapohisi kuna ukiukwaji mkubwa wa uwajibikaji na ufuatilie
- watambue, wasifu na kuwasaidia wawakilishi na viongozi wanaowajibika

## Maswali kwa ajili ya majadiliano

- Je kuna utamaduni na utaratibu wa uwajibikaji wa umma katika jamii yako? Au shule yako?
- Je viongozi wote wanawajibika, au kuna baadhi yao hawawajibiki vya kutosha ukilinganisha na wengine? Hao ni akina nani? Kwa nini hali iko hivyo?
- Wajumbe wa kamati ya shule yako wanawajibika vipi kwa umma? Kwa wanafunzi? Kwa walimu?
- Je una mfano wowote mzuri wa uwajibikaji katika shule yako? Nini kilifanya jambo hilo liwe zuri na liliisaidia vipi jamii?
- Je una mfano wowote ambapo kukosekana kwa uwajibikaji kuliathiri maendeleo? Nini kinaweza kufanyika kuboresha hali hiyo?
- Je ni kwa vipi watu katika jumuiya ya shule – wanafunzi, wazazi na walimu – wanaweza kuchangia katika kuleta uwajibikaji wenye ufanisi?

# Uwazi




## Uwazi ni nini?

- kuchangia taarifa kuhusu sera za elimu na mambo yanayofanyika shuleni ikiwa ni pamoja na matumizi ya fedha
- kuwa wazi kabisa na kuelewa kikamilifu yale yote yanayofanyika shuleni, bila kuficha au kubania taarifa muhimu kwa makusudi
- watu kufahamu ni maamuzi gani yamefanyika na sababu za kufanyika kwa maamuzi hayo
- taarifa zilizo wazi na bayana kuhusu masuala muhimu, zinaandaliwa mara kwa mara na kuchangiwa na wote
- kusambazwa kwa taarifa kwa njia ambayo itawafikia watu kwa urahisi na kwa muundo utakaowawezesha waielewe taarifa hiyo kwa urahisi

- kuwa mwaminifu
- kutoa na kupokea mrejesho kutoka kwa yeyote anayehitaji taarifa hizo
- kujibu maswali kwa ufasaha na ukamilifu
- kuwa na mahali au njia ambazo wananchi wataamini kuwa zitawapatia taarifa zote muhimu watakazozihitaji

## Kinyume cha uwazi ni nini?

- kukosekana kwa taarifa au kutoa taarifa zilizopitwa na wakati
- kutumia taarifa zisizo fasaha au zilizo ngumu kueleweka
- kutumia taarifa za uongo na upotoshaji
- kutoa taarifa kwa wachache tu, bila kuwa na sababu nzuri na za msingi
- kuwepo fursa na nafasi finyu ya kuuliza maswali na kupata majibu yaliyo fasaha
- viongozi kutokujibu maombi ya taarifa kwa wakati unaotakiwa na kwa uwazi
- urasimu na taratibu zenye utata

## Unaweza kufanya nini ili kukuza uwazi?

- tafuta mahali unapoweza kupata ripoti na nyaraka za sera, pata nyaraka hizo na shirikisha wengine
- soma mihutasari ya vikao vya kamati za shule, wahimize wengine wafanye vivyo hivyo na jadili masuala yaliyojitokeza
- changia taarifa na wengine
- tambua mambo ambayo una haki kuyafahamu na dai kufahamishwa kuhusu mambo hayo

- jitolee kusaidia shule iweze kusambaza kwa watu wengi zaidi taarifa zake mbalimbali, hii ikiwa ni kwa kupitia maonyesho ya wazi na katika kuta na mbao za matangazo
- saidia shule iweze kuandaa taarifa zake katika njia itakayowawezesha watu kuzielewa kwa urahisi
- tafuta, himiza na endeleza mifano mizuri ya uwazi katika elimu pamoja na manufaa yake
- toa taarifa/habari kuhusu masuala mbalimbali yanayogusa umma kwa redio, televisheni, magazeti na vyombo vingine vya habari
- Saidia viongozi kuwa na wajibu wa kuchangia habari na wananchi bila hata ya kuombwa kufanya hivyo

**Maswali kwa ajili ya majadiliano**

- Je kuna uwazi shuleni kwako? Je watu wote wanafursa na uwezo wa kupata taarifa muhimu kirahisi, au kuna baadhi ya watu wanaonyimwa taarifa? Hao ni akina nani?
- Je wewe na wengine mnafahamu kuhusu fedha za shule? Je mapato, matumizi na masalio yanatolewa taarifa kwa njia ambayo kila mmoja anaweza kufahamu ni nini kinachoendelea?
- Je taarifa zinachangiwa kwa ufasaha na kwa njia inayowawezesha watu kuzielewa kwa urahisi? Je taarifa zinachangiwaje?
- Je mihutasari ya vikao vya kamati ya shule, mipango ya shule na taarifa za fedha zinapatikana kwa wahusika wote, ikiwemo wanafunzi na wazazi?
- Je kuna mifumo na nyenzo gani nyingine za kuhakikisha uwazi katika kamati za shule na katika jamii?

- Je unafahamu mfano mzuri wa uwazi kwa vitendo? Uliisadia vipi jamii yako?


- Je una mfano wa hali au tukio ambapo kukosekana kwa uwazi kuliathiri maendeleo? Ni nani aliyekuwa akipinga kuwepo kwa uwazi na kwa nini? Nini kinaweza kufanyika ili kuboresha hali hiyo?

- Ni mambo gani yanayoathiri uwazi

- Je serikali inaendeleza na kukuza uwazi? Inaweza kufanya nini ili kuboresha hali iliyopo?

- Je ni rahisi kwa watu mbalimbali (wanaume, wanawake, watoto, masikini, matajiri, watu wenye ulemavu, nk) kuuliza maswali kuhusu masuala nyeti? Je viongozi hujibu vipi maswali hayo?

# Demokrasia




## Demokrasia ni nini?

- mfumo wa utawala ambao huwawezesha watu kuchangia mamlaka na uongozi; na wananchi kuona kuwa wanaweza kuleta mabadiliko
- ushiriki huru bila kulazimishwa kufanya jambo pasipo hiari
- utaratibu wa kufanya maamuzi unaosikiliza na kushughulikia dukuduku, kero na matatizo ya watu mbalimbali, hususan wale ambao kwa kawaida wanatengwa (mfano masikini, vijana, watu wenye ulemavu, na watu wanaoishi na VVU/UKIMWI)
- maamuzi yanayotokana na maoni ya walio wengi na kuheshimu na kuwalinda wachache

- uwazi na haki katika uchaguzi wa viongozi na wawakilishi
- zaidi ya uchaguzi, ni utamaduni endelevu wa wawakilishi kupata mamlaka kutoka kwa wananchi na kutoa taarifa kwa wananchi
- uwajibikaji wa viongozi kwa watu

## Nini si demokrasia?

- kukosekana kwa fursa ya maana na ya kutosha kwa watu kuchangia maoni, mawazo na dukuduku zao, na mambo hayo kutotiliwa maanani
- maamuzi kufanywa na mtu mmoja au kikundi kidogo cha watu kwa ajili ya watu wengine, bila kupata ridhaa na mamlaka kutoka kwa watu hao
- mfumo mbaya wa kuchagua (na kuwaondoa katika mamlaka) viongozi na wawakilishi
- kukosekana kwa taratibu na fursa za kuwawajibisha viongozi kwa wakati wote
- baadhi ya watu kuongea sana na kunyima fursa na haki ya wengine kusikilizwa
- 'utawala wa kundi' ambapo walio wengi wanafanya maamuzi yanayowabagua na kuwanyima haki wachache
- kukosekana kwa taarifa na uwazi

## Unaweza kufanya nini kukuza na kuendeleza demokrasia?

- jadili na marafiki, wenzako na viongozi kuhusu demokrasia, ina maanisha nini kwako na ni kwa jinsi gani itaendelezwa shuleni
- chunguza sera za Serikali (mfano, MMEM na kiambatanisho chake cha *Uimarishaji wa Muundo wa Kitaasisi*) zinasema nini kuhusu kamati za shule zinavyoweza kuchaguliwa na kuendeshwa
- tathmini kiwango cha utendaji wa kidemokrasia cha kamati ya shule

yako na changia taarifa hii na wengine.

- wasiliana mara kwa mara na wajumbe wa kamati ya shule, mwalimu mkuu na viongozi wengine na toa mapendekezo yako kuhusu namna ambavyo demokrasia inaweza kuimarishwa
- chukua muda kuwasikiliza wale ambao kwa kawaida huwekwa pembezoni, wasaidie ili waweze kushiriki kikamilifu na maoni yao yaweze kusikilizwa na watoa maamuzi
- shiriki katika uchaguzi wa kidemokrasia wa wajumbe wa kamati ya shule
- wasiliana na mamlaka zinazohusika pale unapoona ukiukwaji mkubwa wa mchakato na taratibu za kidemokrasia

## Maswali kwa ajili ya majadiliano

- Je shule yako ni ya kidemokrasia? Je kamati ya shule yako ni ya kidemokrasia? Je darasa lako? Je menejimenti/uongozi wa shule? Je hatua za kinidhamu zinazochukuliwa? Ni kwa vipi ni za kidemokrasia na ni kwa kiwango gani?

- Je kuna baadhi ya watu wanaobaguliwa zaidi kuliko wengine? Hao ni akina nani? Watoto? Wasichana? Watu wenye ulemavu? Watu wanaoishi na VVU/UKIMWI? Unaweza kufanya nini ili kuwasaidia?

- Kamati ya shule yako inaendeshaje shughuli zake? Kila mmoja anapata fursa sawa ya kutoa sauti yake? Je viongozi wa kamati wana tawala na kudhibiti vikao au wanampa kila mmoja fursa ya kuchangia kwa haki?

- Wajumbe wa kamati yako ya shule walichaguliwaje? Je wanawajibika kivitendo kwa nani?

- Je una mfano mzuri wa jambo lililofanyika kidemokrasia? Ni nini kilifanya jambo hilo kuwa zuri na ni kwa namna gani liliisaidia jamii yako?

- Je una mfano wa hali au tukio ambapo kukosekana kwa utamaduni wa kidemokrasia kuliathiri maendeleo? Nini kinaweza kufanyika kuboresha hali hiyo?

- Ni mambo gani yanakwamisha au kupunguza kasi ya kujenga utamaduni wa kidemokrasia? Ni mazingira gani yanahitajika kuwa na utamaduni na utendaji wa kidemokrasia iliyokomaa?

- Je Serikali inakuza na kuendeleza kwa vitendo demokrasia? Je inaweza kufanya nini kuboresha hali iliyopo?

# Hitimisho




Kijitabu hiki kimeainisha nafasi muhimu ya kamati za shule katika mageuzi ya elimu yanayoendelea hivi sasa. Kimejadili misingi mikuu mitano inayohitajika katika muundo wa kamati hizo na utekelezaji wa majukumu yake. Kimeandikwa katika mtindo unaolenga kutoa ufafanuzi bayana wa dhana kuu zinazozungumziwa na kuchochea majadiliano kuhusu maana zake, umuhimu wake na nini kinaweza kufanyika katika kuleta mabadiliko ya kweli katika shule zetu.

Kijitabu hiki hakitoi maelezo ya msingi juu ya kanuni, taratibu na majukumu ya kamati za shule. Mambo hayo huandaliwa na Serikali na watendaji wengine. Kwa taarifa zaidi tunakushauri kuyapitia na kuyasoma machapisho yaliyoorodheshwa sehemu ya mwisho ya kijitabu hiki.

Kwa kutegemea zinavyofanya kazi, kamati za shule zinaweza kuwa vyombo

imara vyenye kuwajengea watu ari na hamasa ya kuleta mabadiliko, au kuwa vyombo vyenye kuudhi, dhaifu na vinyonge. Kihistoria, kamati nyingi za shule zimeshindwa kuzitia shule uhai mpya au kuzisimamia vyema na kwa ufanisi. Lakini mageuzi ya hivi sasa yanayofanywa na Serikali, ikiwa ni pamoja na MMEM, yanatoa fursa dhahiri na mwafaka kwa kamati za shule kupata taarifa na kuongezewa uwezo, kuchukua hatua mathubuti na sahihi bila kusubiri kusukumwa au kuagizwa na kufanya mambo yaende. Hii ni fursa nzuri kwa wananchi kuhamasisha, kuchukua hatua na kuboresha elimu na demokrasia nchini Tanzania.

Nawe msomaji, ni sehemu muhimu ya jibu. Mabadiliko na maendeleo hayataletwa kwetu kutoka nje na Serikali, wafadhili au watu wengine. Bali yatakuja pale wananchi watakapoamka, kujiamini, kujipanga vyema na kujenga dhamira ya dhati ya kuleta mabadiliko.

Je utafanya nini kuifanya kamati yako ya shule kuwa mahali pazuri pa kuvutia kwa wote? Je utafanya nini kuhakikisha kamati ya shule yako inafanya kazi ili shule yako iwe bora zaidi?

# Vyanzo na Machapisho Mbalimbali


Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania (URT), *Mkakati wa Kuondoa Umasikini (MKU),* Dar es Salaam, 2001

Miongozo ya ADEM (Agency for Development Education Management), *Kujenga na Kuendeleza Uwezo wa Kamati za shule* (hakuna tarehe)

Mradi wa PAMOJA mkoani Kilimanjaro: *Taarifa ya Utafiti wa Kubainisha Mahitaji ya Kujengewa Uwezo ya Kamati za Shule-Ripoti ya Mwisho,* Moshi, Februari 2002

Program ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu (ESDP), Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM), *Uimarishaji wa Taratibu za Kitaasisi,* Agosti 3 2001

Tanzania Education Network/Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET), *Kamati ya Kuendeleza na Kujenga Uwezo, HakiElimu Working Paper*, 2003

Tanzania Education Network/Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET), *Simple Guide to Working on Finances and Education,* Dar es Salaam 2003

Tanzania Education Network/Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET), *Warsha ya Kujenga na Kuendeleza Uwezo wa Kamati za Shule,* 9-11 Aprili 2002

Wizara ya Elimu na Utamaduni/UNICEF, *Mwongozo wa Mafunzo kwa Wajumbe wa Kamati za Shule,* 1998

Kwa mujibu wa sheria, kila shule ya msingi nchini Tanzania inatakiwa isimamiwe na kuendeshwa na kamati ya shule. Kijitabu hiki kinalenga kusaidia jitihada za Serikali katika kuimarisha kamati za shule na kupanua njia ambazo wananchi wanaweza kuchangia katika kuboresha elimu.

Kijitabu hiki si muongozo wa namna ya kuendesha kamati za shule. Hakionyeshi nafasi, wajibu, kanuni na taratibu zote zinazohusika katika uendeshaji wa kamati za shule. Badala yake, kinaelezea misingi mikuu ambayo itaongoza kamati za shule na wajumbe wake. Misingi hiyo ni haki za binadamu, ushiriki, uwajibikaji, uwazi na demokrasia. Ni muhimu kuijadili na kuielewa vyema misingi hii, kwa sababu kamati yoyote ya shule itakayoshindwa kuizingatia itashindwa kuwa na ufanisi, na hivyo kujiweka katika hatari ya kupoteza imani yake kwa wananchi.




HakiElimu ni shirika la hiari linalolenga kufikia usawa, ubora, haki na demokrasia katika elimu na jamii. Tunafanya hivyo kwa kuwezesha jamii kupata habari, kubadili shule na mfumo wa uundaji wa sera; kuchochea ubunifu wa mijadala ya umma; kufanya utafiti yakinifu, uchambuzi wa sera na utetezi na kushirikiana na wadau ili kuendeleza manufaa ya pamoja na kuzingatia haki za jamii

hakielimu

739 Barabara ya Mathuradas • Upanga
SLP 79401 • Dar es Salaam • Tanzania
Barua pepe: info@hakielimu.org • Tovuti: www.hakielimu.org
Simu: (255 22) 2151852 au 3 • Faksi: (255 22) 2152449